

Soma Biblia kwa Mwaka



- Na Mch. Marek P. Zabriskie, Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la
Christ Church Greenwich (Connecticut), Mwanzilishi wa Kituo cha
Masomo ya Biblia na Changamoto ya Biblia.
www.thecenterforbiblicalstudies.org



Kituo cha Masomo ya Biblia kimeunda ratiba ya kujisomea ya kipindi cha mwaka mmoja ili kusaidia wale waliojitoa ikiwa ni mtu mmoja au waumini wa kanisa, shule ya kanisa au dayosisi kufanikiwa kuisoma biblia yote ndani ya mwaka mmoja. Makusudi ya CBS yamelenga katika kuisoma biblia yote, kusoma vitabu vya biblia kwa mpangilio na kuhakikisha kwamba Zaburi na sehemu ya agano jipya ili kuwapa nguvu za kiroho kila siku na kuwawezesha wasomaji kuweza kuisoma biblia yote.

Unaweza kuanza ratiba hii tarehe 1 mwezi wa kwanza au siku yeyote ya mwaka utakayoipenda. Ratiba hii hufanyakazi vyema kama utaianza jumatatu sababu tunawahamasisha wasomaji kusoma vipande vya biblia jumatatu mpaka jumamosi na tukihisi kwamba jumapili watakuwa kanisani wakisikiliza masomo yasomwayo kwa sauti. Biblia hueleweka vyema katika mazingira ya jamii ya waaminio na kwa mtu ambaye wamejitoa kufuata mafundisho ya Yesu na kufuata maneno ya Mungu katika maisha yao ya kila siku. Usikilizaji wa masomo ya jumapili hata hivyo hautoshi kufahamu na kutambua uzima, Neno la Mungu liletalo mabadiliko maishani.

Tunakuhimiza kila siku kujiweka katika uwepo wa Mungu kabla hujaanza kusoma masomo. Soma ukiwa na hamu ya kuelewa na kufuata mafundisho ya masomo ili maisha yako yaweze kubadilishwa na roho mtakatifu afanyaye kazi ndani yako kama Neno la Mungu lilivyojifunua moyoni mwako, akilini na nafsini. Tunakutakia baraka zote katika uaminifu wako wa kusoma Biblia kila siku.

Tunakupa sala hii iliyoandikwa na aliyekuwa Askofu mkuu Thomas Cranmer mwaka 1549 katika kitabu cha sala kwa watu wote unapoanza safari yako ya kiroho na Changamoto ya Biblia.

“Bwana mbarikiwa aliyefanya maandiko matakatifu yote yaandikwe ili tujifunze, Utujalie ili tuyasikilize, tuyasome, tuzingatie, tujifunze na kwa ndani tuyayeyushe kama chakula, kwamba tuyakumbatie na daima kushika kwa uthabiti tumaini lenye baraka la uzima wa milele ambalo umetupa katika mokozi wetu Yesu; aishiye na kumiliki pamoja nawe na roho mtakatifu, Mungu mmoja, milele na milele. amin.”

Siku ya 1-Mwanzo 1-3; Zaburi 1; Mathayo 1

Siku ya 2-Mwanzo 4-6; Zaburi 2; Mathayo 2

Siku ya 3-Mwanzo 7-9; Zaburi 3; Mathayo 3

Siku ya 4- Mwanzo 10-12; Zaburi 4; Mathayo 4

Siku ya 5-Mwanzo 13-15; Zaburi 5; Mathayo 5

Siku ya 6-Mwanzo 16-18; Zaburi 6; Mathayo 6

Siku ya 7-furahia kusikiliza maandiko matakatifu yasomwayo kwa sauti kanisani.

Siku ya 8-Mwanzo 19-21; Zaburi 7; Mathayo 7
Siku ya 9-Mwanzo 22-24; Zaburi 8; Mathayo 8
Siku ya 10-Mwanzo 25-27; Zaburi 9; Mathayo 9
Siku ya 11-Mwanzo 28-30; Zaburi 10; Mathayo 10
Siku ya 12-Mwanzo 31-33; Zaburi 11; Mathayo 11
Siku ya 13- Mwanzo 34-36; Zaburi 12; Mathayo 12
Siku ya 14-furahia kusikiliza maandiko matakatifu yasomwayo kwa sauti kanisani.

Siku ya 15-Mwanzo 37-39; Zaburi 13; Mathayo 13
Siku ya 16-Mwanzo 40-42; Zaburi 14; Mathayo 14
Siku ya 17-Mwanzo 43-45; Zaburi 15; Mathayo 15
Siku ya 18-Mwanzo 46-48; Zaburi 16; Mathayo 16
Siku ya 19-Mwanzo 49-50; Zaburi 17; Mathayo 17
Siku ya 20-Kutoka 1-3; Zaburi 18:1-20; Mathayo 18
Siku ya 21- furahia kusikiliza maandiko matakatifu yasomwayo kwa sauti kanisani.

Siku ya 22-Kutoka 4-6; Zaburi 18:21-50; Mathayo 19
Siku ya 23-Kutoka 7-9; Zaburi 19; Mathayo 20
Siku ya 24- Kutoka 10-12; Zaburi 20; Mathayo 21
Siku ya 25-Kutoka 13-15; Zaburi 21; Mathayo 22
Siku ya 26-Kutoka 16-18; Zaburi 22; Mathayo 23
Siku ya 27-kutoka 19-21; Zaburi 23; Mathayo 24
Siku ya 28- furahia kusikiliza maandiko matakatifu yasomwayo kwa sauti kanisani.

Siku ya 29-Kutoka 22-24;Zaburi 24; Mathayo 25
Siku ya 30-Kutoka 25-27; Zabuuri 25; Mathayo 26
Siku ya 31-Kutoka 28-30; Zaburi 26; Mathayo 27
Siku ya 32-Kutoka 31-33; Zaburi 27; Mathayo 28
Siky ya 33- kutoka 32-36; Zaburi 28; Mathayo 1
Siku ya 34-kutoka37-39; Zaburi 29; Marko 2
Siku ya 35-furahia kusikiliza maandiko matakatifu yasomwayo kwa sauti kanisani.

Siku ya 36-Kutoka 40; Zaburi 30; Marko 3
Siku ya 37-Mambo ya Walawi 1-3;Zaburi 31; Marko 4
Siku ya 38-Mambo ya Walawi 4-6; Zaburi 32; Marko 5
Siku ya 39-Mambo ya walawi 7-9; Zaburi 33; Marko 6
Siku ya 40-Mambo ya Walawi 10-12; Zaburi 34; Marko 7
Siku ya 41-Mambo ya Walawi 13-15; Zaburi 35; Marko 8
Siku ya 42-furahia kusikiliza maandiko matakatifu yasomwayo kwa sauti kanisani.

Siku ya 43-Mambo ya Walawi 16-18; Zaburi 36; Marko 9
Siku ya 44-Mambo ya Walawi 19-21; Zaburi 37:1-18; Marko 10

Siku ya 45-Mambo ya Walawi 22-24; Zaburi 37:19-42; Marko 11
Siku ya 46-Mambo ya Walawi 25-27; Zaburi 38; Marko 12
Siku ya 47-hakuna somo lililoandaliwa katika siku hii. Tafadhary chagua kurasa uipendayo kutoka kwenye vitabu vya mwanzo vitatu vya agano la kale; Zaburi 39; Marko 13
Siku ya 48-Hesabu 1-3; Zaburi 40; Marko 14
Siku 49-furahia kusikiliza maandiko matakatifu yasomwayo kwa sauti kanisani.

Siku ya 50-Hesabu 4-5; Zaburi 41; Marko 15
Siku ya 51-Hesabu 6-8; Zaburi 42; Marko 16
Siku ya 52-Hesabu 9-11; Zaburi 43; Luka 1
Siku ya 53-Hesabu 12-14; Zaburi 44; Luka 2
Siku ya 54- Hesabu 15-17; Zaburi 45; Luka 3
Siku ya 55-Hesabu 18-20; Zaburi 46; Luka 4
Siku ya 56- furaha kusikiliza maandiko matakatifu yasomwayo kwa sauti kanisani.

Siku ya 57-Hesabu 21-23; Zaburi 47; Luka 5
Siku ya 58-Hesabu 24-26; Zaburi 48; Luka 6
Siku ya 59-Hesabu 27-29; Zaburi 49; Luka 7
Siku ya 60-Hesabu 30-32; Zaburi 50; Luka 8
Siku ya 61-Hesabu 33-35; Zaburi 51; Luka 9
Siku ya 62-Hesabu 36; Zaburi 52; Luka 10
Siku ya 63- furahia kusikiliza maandiko matakatifu yasomwayo kwa sauti kanisani

Siku ya 64-Kumbukumbu la Torati 1-3; Zaburi 53; Luka 11
Siku ya 65-Kumbukumbu la Torati 4-6; Zaburi 54; Luka 12
Siku ya 66-Kumbukumbu la Torati 7-9; Zaburi 55; Luka 13
Siku ya 67-Kumbukumbu la Torati 10-12; Zaburi 56; Luka 14
Siku ya 68-Kumbukumbu la Torati 13-15; Zaburi 57; Luka 15
Siku ya 69-Kumbukumbu la Torati 16-18; Zaburi 58; Luka 16
Siku ya 70-furahia kusikiliza maandiko matakatifu yasomwayo kwa sauti kanisani.

Siku ya 71-Kumbukumbu la Torati 19-21; Zaburi 59; Luka 17
Siku ya 72-Kumbukumbu la Torati 22-24; Zaburi 60; Luka 18
Siku ya 73-Kumbukumbu la Torati 25-27; Zaburi 61; Luka 19
Siku ya 74-Kumbukumbu la Torati 28-30; Zaburi 62; Luka 20
Siku ya 75-Kumbukumbu la Torati 31-33; Zaburi 63; Luka 21
Siku ya 76-Kumbukumbu la Torati 34; Zaburi 64; Luka 22
Siku ya 77-furahia kusikiliza maandiko matakatifu yasomwayo kwa sauti kanisani.

- Watu wengine hufurahia kusoma masimulizi, mkusanyiko wa masimulizi ya biblia uliochapishwa na Zondervan ambao unaacha nasaba na kanuni za

vyakula,n.k. hii ni rahisi kwa watu ambao hawajazoea kusoma biblia lakini si biblia kamili na hili sio chaguo la kwanza kwetu katika mapendekezo.

Kusoma na watoto na masomo kwa vijana

- Tunashauri utumiaji wa biblia kwa kuthamini umri wa watoto pale wazazi na watoto wasomapo biblia pamoja.
- Tafadhali angalia ushauri wa masomo kwa vijana katika “sehemu ya shauri” ya tovuti yetu juu ya “vijana, vijana na familia.”

Unawezaje kunasihi kwamba ninaanza kusoma biblia?

- Tunapinga sana washiriki katika kuisoma Biblia kurasa hadi kurasa kuanzia kitabu cha Mwanzo na kuishia kitabu cha Ufunuo, kwa sababu wasomaji wengi wanaofanya hivi hushindwa kusoma mpaka mwisho. Kuna sehemu nyingi za maandiko ya Waebrania ambazo msomaji atapata changamoto na kukaushwa kiroho na kukata tama ya kuimaliza biblia.
- Tunakuhimiza kusoma sura tatu za Agano la Kale, sura moja ya Zaburi na sura moja ya Agano Jipya kila siku. Hii itakusaikia kuisoma Biblia yote ndani ya mwaka. Kusoma sura ya Agano Jipya na Zaburi kila siku itakuhimili katika kukaushwa kiroho na maandiko ya Waebrania.
- Tovuti yetu itakupa ratiba ya masomo kwa wale wanaotaka kufuata mpango sahihi wa usomaji Biblia kila siku, ambao utakusaidia kuhitimisha usomaji ndani ya muda wa mwaka. Tafadhari angalia “masomo ya mwaka” katika “shauri” sehemu ya tovuti.
- Sababu Biblia si gazeti la habari, ni vima kuisoma kwa unyenyekevu wa kiroho. Tunapigania kuikaribia kwa moyo wa ibada kwa kuisoma Biblia kuliko kuisoma kama msomi safi au zoezi la kielimu. Tunakusisitiza kuanza kila kipindi kwa kujiweka mwenyewe katika uwepo wa Mungu pale uanzapo kusoma.
- Tunapenda mwenendo wa utawa wa kale wa *lectio divina*, ambapo unasoma maandiko, na kuitafakari sehemu hiyo, kisha unamuomba Mungu na unasikiliza kwa utulivu kwa majibu ya Mungu. Kwahiyo tunasisitiza wasomaji wote kuisoma biblia kwa maombi.
- Tunakuhimiza kusoma asubuhi kwa dakika 20 au 30, Usomaji wako wakimaombi utakuchangamsha kiroho katika siku zilizobakia. Kama huwezi kusoma asubuhi, soma pale uwezapo baadae katika siku, hasa kama utakuwa nje ya muda wa kawaida wa kujisomea.
- Tunakuhimiza kupitia kwa haraka, kuengua au kuruka nasaba zilizo ndefu, maelezo marefu ya ephod au ujenzi wa hekaru, dhabihu za wanyama au kanuni za

vyakula zinazopatikana katika maandiko ya Waebrania. Pata mambo muhimu na endelea mbele ili uweze kubaki na kazi ya kumaliza kusoma Biblia.

